# UBANDIKAJI MAJINA NA MAJUMLISHI MEMETO KAMA MIKAKATI YA PROPAGANDA KATIKA MDAHALO WA URAIS WA KENYA 2013

**Khaisie J. L.Wanyama**
**Wandera P. Simwa**
&
**Mayaka J. Gwachi**
*Idara ya Masomo ya Kifasihi na Mawasiliano*
Chuo Kikuu cha Laikipia,
Nyahururu, Kenya

*IKISIRI*

*Wanasiasa hutumia mbinu anuai kuelekeza uelewa wa suala la kisiasa; mikakati ya propaganda haswa ndiyo hutumika zaidi katika kampeni za kisiasa miongoni mwa wanadamu wote ulimwenguni. Shida kubwa ni kama jamii ya kistarabu na kibinadamu inaweza kuendelea kuthamini na kushiriki katika propaganda katika shughuli za uteuzi wa uongozi: kwani kwenye propaganda huwa kupiga chuku,uongo, chuki na mambo mengi ambayo ni kinyume na kutangamana kwa wanadamu kama washiriki wenza katika jamii. Kazi hii imetathmini namna mikakati miwili ilitumiwa na wagombea wa kiti cha urais nchini Kenya, mwaka wa 2013, kwa lengo la kushawishi wapiga kura na kujipa umaarufu. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Matini. Data ilikuwa kauli zilizoingiana na mikakati ya propaganda. Uchanganuzi ulizingatia maarifa ya kithamani, ya kimaudhui na kiuhakiki. Matokeo yalionyesha matumizi ya ubandikaji majina na majumlishi memeto. Tekniki hizi zilitumiwa na wagombea kwa lengo la kujijengea sifa njema huku wakilenga kubomoa sifa za wapinzani. Pia zilitumiwa kwa dhamira ya kuuza sera za vyama vyao huku wakidhamiria kudhalilisha sera za wapinzani. Kazi hii ni mchango adimu kwa taaluma ya uchanganuzi matini na mawasiliano ya kisiasa. Aidha ni ya manufaa kwa wanafunzi wa uchanganuzi matini, sayansi ya siasa na mawasiliano. Tafiti zaidi zinaweza kufanywa kuhusu mbinu nyingine kama vile balagha, na pia kuzingatia nadharia zingine tofauti zinazohusu uchanganuzi wa matini.*

***Istilahi maalumu:*** *Propaganda, ubandikaji majina, majumlishi memeto, balagha, Uchanfanuzi hakiki wa Matini, maarifa ya kithamani, maarifa ya kimaudhui, maarifa ya kiuhakiki*

## Utangulizi

Kampeni za kisiasa hutumiwa kueneza habari muhimu zinazowawezesha wapiga kura kufanya uteuzi wa busara kupitia haki yao ya kupiga kura. Mgombea hupata fursa ya kuwashawishi wapiga kura kumkubali kuchukua hatamu za uongozi. Pia hudhihirisha kuwa mgombea anayo maadili yanayomhusu anayetaka kuwa kiongozi (Benoit 2009). Vilevile huweza kuathiri namna wapiga kura huwatazama wagombea na hata kubadili mielekeo ya wapiga kura.

Marekani ndiyo nchi yenye historia ndefu ya kuandaa midahalo ya kampeni za urais. Ndiyo inayojulikana sana na yenye umaarufu mkubwa kote duniani (Pekka 2011). Hata hivyo tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu midahalo hiyo zimekuwa zikilenga zaidi kipengele cha maudhui na athari ya midahalo hiyo kwa upigaji kura kuliko kipengele cha lugha, hasa matumizi ya mikakati ya propaganda.

Matumizi ya mbinu ya balagha kuundia simulizi, na nchi za Magharibi kumfafanua Saddam Hussein wa Iraq, pamoja na kuelezea vita vya Bosnia, ni mifano mizuri ya namna ya kutumia lugha kusimulia hadithi nzuri ili kufikia malengo ya kisiasa (Uvehammer 2005). Uchanganuzi wa lugha ya propaganda na namna ilivyotumiwa na uongozi wa Hitler dhidi ya Wayahudi ili kuzua chuki, ubaguzi wa kimbari na kupotosha ukweli na uhalisia, ni mfano tosha.

Kampeni za kisiasa nchini Kenya zimechukua mielekeo ya mataifa mengine ambayo yanazingatia mfumo wa demokrasia. Kumeshuhudiwa utaalamishaji wa mawasiliano ya

kisiasa; tena vyama na wanasiasa binafsi wameangazia umuhimu wa vyombo vya habari katika mawasiliano ya kisiasa na msisimko unaohusiana na kampeni.

Nchini Kenya kampeni zimedhihirisha matumizi ya mbinu kama upachikaji majina na hata istiara. Wanasiasa hutumia lugha kuharibiana sifa, kutupiana matope na kutoleana vitisho. Yote haya hulenga kuibua athari za aina tofauti tofauti kwa wagombea wenza na kwa hadhira (Irungu 1999).

Ni wakati mwafaka kwa wapiga kura kuwa na uwezo wa kupenya, kutathmini na kuhakiki jumbe zinazowasilishwa kwao ili wasiwe tu wa kufunda na kumeza kila kitu kinachosemwa na wanasiasa. Umma unahitaji kuwezeshwa kuchuja kila jumbe ili kupata maarifa kuhusu ulimwengu unaouzunguka na kujiundia mitizamo yao binafsi (Smith 2003). Ni kutokana na misingi hii ndipo wasomi wakahitari kutekeleza uchunguzi na kuandika makala haya.

## 1. Mapitio ya Maandishi

Irungu (1999) alichunguza sanaa ya hila za kisiasa za Kenya. Alitambua matumizi ya upachikaji majina kwa viongozi, wafuasi na wapinzani. Kazi yake ni muhimu kwa uchunguzi huu kwa kuwa ilitambua kuwa lugha ya kisiasa mara nyingi ni lugha ya hila. Tofauti ni kuwa Irungu hashughulikii moja kwa moja mikakati ya propaganda kwa ukamilifu. Pia kazi ya Irungu ililenga siasa za chama kimoja cha KANU. Kazi hii ilichunguza mdahalo wa urais wa 2013 ambao uliibuka katika siasa za vyama vingi.

Kuusisto (kama anavyonukuliwa katika Uvehammer 2005), alichanganua mbinu ya balagha na vile ilivyotumiwa na viongozi wa nchi za Magharibi katika kuunda na kuelekeza simulizi kuhusu mitafaruku iliyotokea miaka ya tisini. Aliangazia vita dhidi ya Saddam Hussein vilivyotokea katika eneo la Ghuba ya Uajemi na mitafaruku kati ya WaSerbia, WaKroatia na Waislamu huko Bosnia Herzegovina. Tasnifu ililenga kutambua namna maana na uaminikaji unavyojengwa kwenye sera za kigeni katika muktadha wa vita. Ilisisitiza kuwa viongozi wa nchi za Magharibi walioungana dhidi ya Hussein walitoa matamshi na kauli zilizolenga kuhalalisha vita, wakaviita 'vita vya haki' vilivyonuia kuukomboa ulimwengu kutoka kwa mikono ya dhalimu. Kinyume ni kuwa, vita vya Bosnia vilichorwa kama vita vya kikatili, visivyokuwa na maana ila uchinjaji wa kiholela. Hii ni mbinu ya propaganda.

Longe na Ofuani (1996) walidai kuwa azma ya pekee ya propaganda ni kupotosha na kutia kasumba. Walisema propaganda hulenga kupotosha ukweli na mjadala. Mpiga propaganda huficha ukweli muhimu kimakusudi na kuchepua mkondo wa fikra na nadhari ya hadhira. Kazi hii imechanganua vile mikakati miwili ya propaganda ilitumiwa kufikia hili katika mdahalo na  wa urais wa Kenya wa 2013.

Mesthrie na wenzake (2000) walifafanua kuwa vipengele muhimu vya lugha ya propaganda ni matumizi ya lugha ya mazaji, ujengaji wa mahusiano, maana matilaba, uradidi na urahisishaji wa uhalisia. Hii ni mbinu ambayo hutumiwa na serikali, hasa za mataifa yaliyostawi. Wakati wa kipindi cha Nazi, lugha ya Kijerumani ilisheheni istilahi za ki-Nazi. Katika propaganda yao maneno "Ujerumani" na "Mfanyakazi" yalitumiwa kama visawe. Kulikuwa na watu wa aina mbili; mfanyakazi mkweli na mwaminifu (mjerumani) dhidi ya mwizi (Myahudi). Hali hii ilipelekea kuzuka kwa chuki ya kimbari na baadaye mauaji ya halaiki ya wayahudi.

Mchango wa Mesthrie ni muhimu kwa kuwa, sambamba na utafiti wa kazi hii, inamulikia jinsi matumizi ya propaganda yaweza kutumiwa kuzua chuki, uchochezi na maovu mengine. Tofauti ni kuwa yeye hapambanui mikakati mbalimbali ya propaganda kama ilivyofanya kazi hii. Vilevile, ni muhimu kwamba kazi hizi mbili ni tofauti katika mukhtadha wa wakati,

mahali na mawanda ya kisiasa.

Oglivy 1963 alichunguza lugha inayotumika katika utangazaji na kutaja baadhi ya sifa ambazo huleta ufanisi mkubwa. Sifa hizo ni "upya", "uhuru", "ajabu", "uzuri" na "ubora wa ziada". Alieleza kuwa lugha ya matangazo hutoa ushawishi kwa kutumia msamiati wa kiutendaji kwa weledi kufanikisha madhumuni mahususi. Kazi ya Oglivy ilifaa kazi hii hasa kwa aina ya lugha ambayo hutumika katika utangazaji na namna inavyoshawishi umma. Oglivy alitaali na kuchunguza lugha kwa jumla, hivyo kuipa kazi hii nafasi ya kuchunguza mikakati mahususi.

Paxon (1985) alizungumzia sheria za mtindo kwa mwandishi wa kibiashara. Alieleza kuwa maneno na maana yapaswa kupewa heshima inayostahili. Hivyo ni kwa kuwa mzungumzaji au mwandishi asipotumia maneno kwa uangalifu, anaweza kusababisha maafa. Kazi ya Paxon ilionyesha umuhimu wa mtindo mwafaka na msamiati faafu katika mawasiliano. Kufaulu kwa mawasiliano hakutegemei tu ujumbe bali pia msamiati bora na mtindo mzuri. Kwa hivyo kazi ya Paxon ilishadidia umuhimu wa utafiti huu. Suala la sheria za mitindo na maneno yenye heshima kutumika ni muhimu kwa kuwa mitindo mibaya na maneno yasio ya heshima aghalabu huzua misukosuko katika kampeni.

Szanto (1978) alifafanua lugha ya siasa kama msamiati wa ushindani na sarakasi, dhihaka na shutuma, mazaji na ushawishi, chuku na kemeo. Alisema ni lugha ya kujasirisha wakereketwa kuangamiza baadhi na kubadili fikra za wengine; ni aina ya sera-chochezi. Ufafanuzi wa Szanto unakaribiana sana na malengo ya watumizi wa mbinu ya propaganda. Wao pia hutumia mikakati ya propaganda kudhihaki, kushutumu, kushawishi na hata kukemea.

## Msingi wa Nadharia

Uchanganuzi huu umeelekezwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Matini iliyoasisiwa na Fairclough na Wodak 1997, wawili hawa wakiwa washiriki wakuu katika kongamano la Amsterdam miaka ya mwanzo ya tisini, karne iliyopita. Nadharia hii imejikita katika mihimili ifuatayo:

- Hutambua umuhimu wa muktadha ambamo lugha hutumika. Inaeleza kuwa mashirika ama watu wanaong'ang'ania mamlaka hutumia lugha kujaribu kuathiri na kushawishi itikadi za jamii ili zifanane ama zikaribie zile wanazotaka ama wanazopendelea.
- Huiona lugha kama tendo la kijamii; hivyo ni lazima matumizi ya lugha yatathminiwe vilivyo. Nadharia inaonyesha vile mahusiano ya kijamii, utambulisho, na nguvu/ mamlaka hudhihirika kupitia lugha.
- Hutambua wanaonyanyaswa katika jamii na kuelekeza nia ya kutaka kuwanasua kutokana na unyanyasaji huo.
- Hufafanua namna mamlaka hujadiliwa na kuelekezwa kupitia diskozi.
- Lugha huchangia katika ubadilikaji wa jamii na utamaduni, yakiwemo mahusiano ya kimamlaka.
- Diskozi/Usemi huzalisha mahusiano ya kimamlaka yasio na usawa, ya kuwanyonya wasio na uwezo.

## Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ni wa aina ya kimaelezo. Aina hii humwezesha mtafiti kubainisha, kueleza au kutambulisha masuala au tatizo la utafiti kupitia data iliyokusanywa kwa nia ya kuliweka wazi ili lieleweke vizuri. Orodho (2003) anasema kuwa ukaguzi wa kimaelezo hutumiwa katika utafiti wa kimaelezo kwa kuwa humpa mtafiti nafasi ya kukusanya data, kuifupisha data, kuiwasilisha na kuifasiri akikusudia kuibainisha na kuiweka wazi.

Njia ya kimakusudi ilitumiwa katika kuteua data ya utafiti huu. Patton (1990) alisema kuwa uwezo wa mantiki katika usampulishaji wa kimakusudi hujihusisha na uchaguzi wa taarifa yenye kadhia nyingi ili kuwezesha mchunguzi kutekeleza utafiti wa kina. Nwandito (1999) anaeleza kuwa njia hii ya kimakusudi ni bora pale mtafiti anaazimia kupata data ya kukidhi kusudi fulani. Gal (1996) naye anadokeza kuwa mtafiti anahitaji kwenda kwenye chanzo cha data bila wasiwasi ikiwa anafahamu kile anachokilenga.

Huu ulikuwa utafiti wa kithamani. Data ya utafiti ilikuwa maneno, virai, sentensi, aya ama kauli zilizotolewa na wagombea wa urais ambazo zilikuwa na sifa za mikakati mbalimbali ya propaganda. Mtafiti alicheza kanda iliyo na rekodi ya mdahalo wa urais wa 2013 na kuisikiliza mara kadhaa na kwa makini. Alitambua kauli na matamko yaliyoingia katika kategoria za mikakati ya propaganda iliyotumiwa na wagombea katika mdahalo. Aliyatenga matamko hayo na kwa kufuata kihesabu-tepu akayanakili kwenye jedwali la kukusanyia data. Data iliyokusanywa ilimwezesha mtafiti kutambulisha mikakati ya propaganda iliyotumiwa na wagombea katika mdahalo.

## Uchanganuzi wa Data

### Mzaha, Kukebehi, na Kubandika Majina

Taasisi ya Uchanganuzi wa Propaganda (1938) inafafanua tekniki ya ubandikaji majina kama mbinu ya kuhusisha mtu au wazo fulani na ishara hasi. Mtumizi wa tekniki hii hufanya hivyo kwa kutumaini kuwa hadhira itamkataa mtu au wazo hilo, kwa msingi wa ishara hasi zilizotumiwa. Badala ya kuzingatia ushahidi uliopo kuhusu jambo, watu huzingatia hisia hasi zinazoibuliwa na maneno au majina yanayotumiwa. Hutumiwa maneno kama 'msaliti', 'mwoga', 'fashisti', 'bwege', 'gaidi', na 'wazimu'. Hulenga kufifiisha sifa njema aliyo nayo mtu, kuchochea hisia za wasikilizaji na hata kutumiwa na wenye nia mbaya kuwatia watu wazimu wa kuchinjana kama hayawani. Ubandikaji majina ambao hutokea kwa wazi zaidi wa matumizi ya dhana za matusi kama vile 'mwizi', 'nguruwe' na 'fisi'.

Lengo kuu la mbinu hii ni kuchocha matendo na maamuzi ya watu kuhusu jambo ama suala bila kupewa fursa ya kufanya utathmini na uchanganuzi wa kina kuhusu suala husika. Hunuia kuwafanya watu kutupilia mbali stadi ya urazini, kudharau ukweli na kuondoa uwezekano wowote wa hadhira kufanya uhakiki wa kina wa suala. Mtumiaji wa tekniki hii hutoa madai bila ya kuyatetea kupitia ushahidi wenye mashiko. Huyabwaga madai kwa nia ya kumbomoa na kumdhalilisha mpinzani.

Uvunjiaji heshima nii mchakato ulio dhamiri na thabiti wenye lengo la kuvunja ustahili na sifa njema ya mtu, taasisi, kundi la wanajamii au taifa. Kama ilivyo na ubandikaji jina, uvunjiaji heshima pia unaweza kujitokeza wazi ama kijanja. Inamhitaji msikilizaji kufikiria sana ili kuelewa kinachosemwa. Mtumiaji hupiga chuku, kuchepua na kupotosha ukweli. Hali hii yaweza kupelekea mlengwa kukataliwa na jamii ama hadhira, kutimuliwa na kutengwa.

### 1.1. Jinsi Mzaha na Kebehi zinavyotokeza

Kenneth anamwita Kenyatta mnyakuzi wa ardhi huku Odinga akimwita fisi ingawa hawafanyi hivyo wazi. Ilianza baada ya msimamizi wa mdahalo kumwomba mgombea Kenneth atetee kauli zake alizodaiwa kutoa huko Voi alipokuwa katika harakati za kampeni:

> *Ulipokuwa ukiendesha kampeni huko Voi ulisema yafuatayo: "Mimi si mnyakuzi wa ardhi kama walivyo baadhi ya washindani wangu. Mie ndiye mgombea wa pekee ninayeweza kutekeleza sera ya kitaifa ya ardhi." Bwana Kenneth, bado unashikilia kuwa baadhi ya wagombea, ama wote, ni wanyakuzi wa ardhi; na utafanya nini kuhusu suala hili kama rais?*
> Msimamizi, Awamu 2 (0:31:50)

Katika jibu lake Kenneth anaonekana kusimama na kutetea madai hayo.

> *Sijawahi kuhusishwa na ugawaji au unyakuzi wa ardhi, huo unabaki ukweli. Kuna kesi ambazo zimesambazwa kuhusu baadhi ya washindani wangu, wanaweza kuthibitisha ... Hata hivyo nafikiri ni muhimu kuwa na mtu mwenye mikono safi wa kutekeleza sera ya kitaifa ya ardhi.*
> Kenneth, Awamu 2 (0:32:20)

Karua anatilia podo suala hili, Awamu 2(0:34:45). Dida, Awamu 2 (0:53:30) anafanya vivyohivyo pia. Lakini mchango wa Odinga ndio unaoshindilia zaidi madai haya:

> *Kuna watu ambao wanagombea uchaguzi huu walio na kesi mahakani. Ndugu yangu hapa (Kenyatta) ana masuala ya kesi kuhusu umiliki wa ardhi. Kuna wengine walio na kesi kwa wizara ya ardhi. Huwezi kuruhusu fisi kulinda mbuzi wako.*
> Odinga, Awamu 2 (0:41:00)

Kwa kumwita Mgombea Uhuru 'mnyakuzi wa ardhi' na 'fisi', Kenneth, Karua Dida na Odinga wametumia tekniki ya propaganda ya ubandikaji jina na uvunjiaji heshima. Wanamsawiri Kenyatta kama mgombea anayetawaliwa na tamaa. Wanamchora kama mtu anayeweza kunyakua hata vya watu maskini bila kujali watakavyoishi hao maskini. Wanataka hadhira iwaamini kuwa huyu Kenyatta ni mtu asiye na utu. Wanahamisha sifa zote za fisi kutoka kwa mnyama huyu na kumtwika Kenyatta. Nia yao kuu ni kumpa ishara hasi ambazo zinachukiwa na wapiga kura na zinazoweza kuwafanya wamchukie kama mgombea. Wanalenga kuchochea hisia za hadhira ili irukie uamuzi utakaowanufaisha wao na kumhasiri Kenyatta.

Hawa wanaomshambulia Kenyatta wanaelewa fika kuwa suala la ardhi huamsha mihemko mikali kila linapotajwa kwa kuwa huhusishwa na dhuluma za kihistoria. Kwa hivyo, wanafahamu kuwa wakilizua suala hili la ardhi katika mdahalo, watazamaji wengi watakimbilia uamuzi bila kwanza kutumia urazini wao kulitathmini pasipo miegemeo. Wanalitumia kuvunja ustahili wa Kenyatta huku wakilenga kujijengea wao. Wanataka hadhira imkatae na kumtenga Kenyatta kwa kumwona kama adui wao, adui wa jamii nzima na hasa adui wa wanyonge ambao huteseka na kutokwa na jasho jingi katika harakati za kutafuta mkate wa kila siku.

Mfano unaofuata unahusu ukabila na wakabila. Ukabila hugawanya na kutenga watu katika makundi mawili; kundi letu 'sisi' (wateule) na kundi lao 'wao' (maadui). Hupuuza na kudharau kila aina ya mantiki. Una uwezo wa kuzagaa katika kila eneo la maisha ya jamii na kudhibiti tabia, mienendo na matendo ya wanajamii kwa kiwango cha kuogofya.

Migogoro, mitafaruku na vita vinavyoshuhudiwa ulimwenguni kote vina mizizi yake katika ukabila. Mauaji ya kimbari, mara nyingi, huwa ni zao la ukabila. Ukabila huchipuka kutokana na imani potovu kwamba, 'kundi letu haliko salama kwa sababu ya kuwepo kwa kundi hilo lingine; na kwa hivyo, ili tuwe salama ni lazima kundi hilo pinzani liangamizwe. Ropeik (2012) anasema kuwa maoni yetu (kama watu binafsi) huundwa kwa namna ambavyo yataoana na yale ya kundi letu bila kujali uhalali wake. Utafiti wa Ropeik umeonyesha kuwa kadiri maoni yetu yanavyoenda kinyume na uhalisia ndivyo tunavyoyategemea zaidi, ndivyo tunavyoyaamini sana na kufunga akili zetu ili tusione maoni badalia (ya wengine). Maoni haya ya Ropeik yanaonyesha vile watu hujikuta katika makundi ambayo baadaye hutambulika kama ya kikabila. Huanaanza kwa kujijengea fikra na maarifa ambayo hayaakisi uhalisia na kisha kuyashikilia kwa imani kuwa ndiyo ya kweli. Ni vigumu kuwabadilisha watu wa aina hii.

Howard (1998) anaongeza kuwa kadiri tunavyoonekana kufadhaika na kuwa na mashaka kuhusu maisha, na kadiri tunavyoonekana kutokuwa na udhibiti wa namna mambo yanavyoenda, ndivyo tunavyozidi kuning'inia kwenye ukabila. Ukabila unakuwa kama ngome ya mwisho ya kukimbilia baada ya kuonekana kutokuwepo njia nyingine ya kusuluhishia matizo yetu ya kibinafsi. Hii ndiyo maana inayojitokeza mgombea anapomwita mpinzani wake mkabila:

> *Mtu akienda kwenye kituo cha kitaifa cha runinga na kuringia tarakimu za kikabila akisema kuwa, kwa sababu mgombea wetu anatoka katika kabila hili, kwa sababu hii, mgombea wetu alishinda kura wakati wa usajili wa wapiga kura. Hili ni tamko hatari kwa kuwa kimsingi anapuuza makabila mengine.*
> Odinga, Awamu1, (0:29:33)

Wakati anamkemea Kenyatta na kundi lake kwa kuwa wakabila na kueneza ukabila, naye Odinga anakemewa na Muite kwa kosa lilo hilo, lakini kijanja.

> *Kwanza kabisa wacha niseme kuwa nimefurahi sana kusikia mheshimiwa Waziri Mkuu (Odinga) akisema kuwa mkarara wa 41 dhidi ya 1 ulibuniwa na vyombo vya habari. Vyombo vya habari hufanya makosa mengi... inahitaji kukemewa zaidi na zaidi.*
> Muite, Awamu 1, (0:46:20)

Wagombea wanaitana wakabila na kulaumiana kwa kutumia ukabila katika kampeni zao. Odinga anamlaumu Kenyatta kwa kuwagawa na kuwatenga Wakenya kwa misingi ya kikabila. Anamlaumu kuwa, anaamini, kwa sababu anatoka katika kabila kubwa, akiliunganisha na lingine kubwa la mwenza wake (Ruto) wanashinda uchaguzi hata kabla ya kura kupigwa. Kenyatta anayapinga madai haya. Muite naye anamlaumu Odinga kwa kutumia mbinu yiyo hiyo katika kampeni ya mwaka wa 2007. Inadaiwa aliyaunganisha makabila arubaini na moja dhidi ya kabila moja, jambo ambalo lilizua uhasama na kupelekea vita vya baada ya uchaguzi. Naye Odinga anapinga madai hayo.

Alipohujumiwa, Uhuru hakunyamaza. Alijitetea. Wagombea hujikinga kwa sababu ya kutaka 'kuokoa uso' na kuzuia mashambulizi zaidi. Pia kujikinga kunasaidia mgombea kurejesha ustahabu wake na imani ya wapiga kura kwake

> *Nafikiri nahitaji kuanza kwa kusema kuwa nitapenda sana mheshimiwa dadangu hapa (Karua) anipeleke kwa hiyo ardhi ... Kwanza kabisa suala la ardhi ni suala la kuamsha mihemko sana nchini Kenya. La kusikitisha ni kuwa namna ambavyo limekuwa likishughulikiwa si kwa njia ya kitaalamu wala ya kutafuta kupata suluhu ... Nimesema wazi ... kila mtu lazima achunguzwe. Kila mtu ambaye amewahi kushtumiwa au kushtakiwa kwa kujihusisha visivyo na masuala ya ardhi,*

*tume ya ardhi lazima umshughulikie, ikianza na mimi. Lakini ningependa kuwakumbusha, mpaka sasa, isipokuwa tu uvumi unaoenezwa, hakuna mtu, hakuna mtu yeyote ambaye amejitokeza kusema na kuonyesha kuwa nimejihusisha visivyofaa na masuala ya ardhi popote nchini.*
Kenyatta, Awamu 2 (0:35:52)

Kupitia jibu lake, Uhuru anazua hoja kadhaa. Kwanza, anahoji kuwa si kweli kuwa amenyakua ardhi yoyote mahali popote. Pili, anaeleza kuwa wanaotoa madai haya hawana ushahidi wowote isipokuwa kutegemea uvumi. Tatu, yuko tayari kuchunguzwa na tume ya ardhi ili athibitishe mbele ya umma kuwa yeye ni mwangavu katika shughuli zake. Mwisho, kupitia jibu hili, anaelekea kuwahakikishia wafuasi wake kuwa madai hayo hayana mashiko na kwa hivyo wayapuuze. Jibu lake linanuia kumlinda dhidi ya hujuma zilizotolewa na wapinzani wake. Anajaribu kuokoa sifa na tabia zake njema zinazotishwa na mahasimu wake.

## Majumlishi Memeto

Majumlishi memeto ni mbinu ya kutumia, kwenye uneni au maandishi, matamko yanayoathiri sana hisia za wasikilizaji na kusababisha hali ya kuhemkwa mno kwa hadhira. Ni mtindo ambao huhusishwa sana na dhanaishi na itikadi zinazosadikiwa na kuenziwa na wanajamii. Brownell (2016) anafafanua majumlishi memeto kama matumizi ya maneno au kauli zibwe ambazo karibu kila mtu huelekea kukubaliana nazo kwa sababu ya namna zinavyoonekana kuwa faafu na zenye thamani. Hata hivyo, ukichunguza, utakuta kuwa hakuna aliye na uhakika kuhusu thamani hiyo au ufaafu wake. Kwa hivyo, ujumlishi na umemeto wake unaishia tu katika hali ya kutoa kauli za kuleta mvuto na msisimko miongoni mwa wasikilizaji bila kuwepo ushahidi wa kutetea na kahalalisha matumizi yake.

Shabo (2005) anaeleza kuwa mwanapropaganda, kwa makusudi, hutumia maneno yenye maana tilaba nzito ili kuumua hisia za hadhira bila kuzitolea ufafanuzi mwafaka. Dhanaishi ambazo hulengwa na wanenaji ni zile ambazo huthaminiwa na kuheshimiwa sana kiasi kwamba zinapotamkwa huvutia uungwaji mkono. Baadhi ya istilahi ambazo hutumiwa sana katika tekniki hii ni 'amani',' umoja' 'uhuru', 'mageuzi', 'usalama', 'demokrasia', 'utamaduni', na 'maendeleo'. Ujuzi huu ukitumiwa vizuri, huweza kumfaidi mgombea kwa namna nyingi zikiwemo; uwezo wa kuathiri moja kwa moja hisia za watu, kuonyesha kuwa mgombea ana maadili mema na anawajali watu wake, na kuwa anayoyasema yanatoka ndani ya roho yake. Aidha mgombea anapata fursa ya kubadili na kuelekeza imani za wasikilizaji kujihusu na kuhusu sera zake. Anakuwa na nafasi ya kujinasibisha na uadilifu anaoweza kuutumia kutafuta uidhinishaji kutoka kwa wapiga kura bila kuwepo mwanya wa kutathminiwa wala kuulizwa kuwajibikia ayasemayo.

Majumlishi memeto hutambulika kwa sifa mbili: kwanza, sifa ya kutokuwa dhahiri na kusababisha ukungukungu katika mawasiliano. Humwacha msikizaji katika hali ya kutokuwa na uhakika wa yale amaanishayo msemaji. Pili, ni sifa ya maana-tilaba chanya. Ni kawaida kwa binadamu wote duniani, bila kujali asili au rangi yao, kupenda kujinasibisha na dhana za aina hii hata kama katika fikira na matendo yao hawakubaliani nazo. Maana zake hubaki kuwa dhahania tu.

### 1.2. Jinsi za Majumlishi Memeto katika Mdahalo

Mfano:

*Katika NARC-Kenya, tu wanademokrasia wa kijamaa. Masuala yaliyo muhimu*

*kwetu ni yale yanayohusu haki za jamii, usawa na kuhakikisha kuwa wanyonge wamelindwa. Masuala ya hadhi ya utu na umoja.*
Karua, Awamu 1, (1:21:38)

Hii kauli ya Karua ni nzuri sana hasa kwa masikio ya wafanyakazi, wanyonge, watoto, wanafunzi, makundi yaliyotengwa na raia wote kwa jumla. Anasema chama chake cha Narc Kenya kinasimamia hayo yote. Swali ni je, anamaanisha anachokisema? Demokrasia ya kijamaa ni itikadi za kisiasa, kijamii na kiuchumi zinazounga mkono uingiliaji kati wa serikali kuimarisha haki za jamii. Huunga mkono kuwepo kwa haki za wafanyakazi kushiriki katika majadiliano yanayohusu masilahi yao ya mahali pa kazi, uwakilishi wa kidemokrasia katika nyanja za maisha, kuwepo kwa mahitaji ya jumla ya raia na ustawi wao kwa upana wake. Sera zake hukamia kusababisha mageuzi ya kuondoa ubepari ambao hudhulumu wasio na uwezo na kupelekea kuzaliwa kwa ujamaa ambao hujali kila mtu kupitia mifanyiko halali ya kisiasa na kisheria. Malengo yake ya hatimaye ni kuwepo kwa usawa, kuondoa unyanyasaji wa wanyonge na kufurusha umaskini. Aidha demokrasia ya kijamaa hupigania kuwepo huduma nzuri ya umma kwa wakongwe, kulindwa kwa haki za watoto, kina mama, huduma nzuri za afya kwa wote, haki za wafanyakazi na elimu ya lazima na nafuu kwa kila raia.

Karua anafahamu kuwa wapiga kura wengi wana mahitaji tumbi. Anaelewa wana utashi wa kusikia na kuona kuwa kuna mgombea anayewajali. Wana hamu kuyasikia hayo yakiahidiwa na wawaniaji. Anajua maneno haya ni wimbo mtamu kwa masikio ya wasikilizaji. Raia wengi wamenyimwa haki ya kushiriki katika majadiliano kuhusu maslahi yao mahali pa kazi. Hawapewi nafasi ya kuamua namna ya kugawa na kutumia rasilmali ya umma. Wengi wao wamepigwa chenga kwa masuala ya afya, elimu na mahitaji ya kimsingi. Kwa sababu hii, wana matamanio ya kuona mageuzi halisi yatakayoleta shufaa katika maisha yao. Karua anamaizi kuwa, hakika, huu ni ujumbe utakaogusa hisia zao.

Anatumia mbinu hii kujitukuza na kuonyesha anajali mahitaji ya wanyonge. Anataka hadhira iamini kuwa anachokisema kinatoka ndani ya roho yake na kwa hivyo imsadiki kuwa ni mgombea anayefaa zaidi kupigiwa kura. Dosari ni kuwa hadhira haina uhakika kama anachokisema ndicho anachokimaanisha na ndicho wanachokielewa wao. Bila kuwepo ushahidi wa kudhihirisha kuwa ana uwezo na nia ya kuyatekeleza yanayosimamiwa na chama chake, umma unakosa njia ya kupimia ukweli wa kauli zake wala namna ya kumfanya kuwajibikia ayasemayo.

Mfano mwingine unamhusu Kenyatta. Anasema:

*Msingi wa muungano wetu ni amani, umoja na maridhiano ya makabila yote katika nchi hii ... Muhimu zaidi nasimamia amani, maridhiano ya kitaifa na umoja.*
Kenyatta, Awamu 1, (1:52:44)

Kenyatta anataja dhana tatu muhimu ambazo humgusa sana Mkenya; dhana ya 'amani', dhana ya 'umoja' na ya 'maridhiano'. Hizi ni dhana ambazo kila mtu hupenda kujihusisha nazo kwa kuwa zinasimamia wema na utulivu katika maisha ya jamii. Amani huwezesha nchi kuendesha shughuli zake vyema. Kuwepo kwake huleta utulivu, ustawi na maendeleo. Amani huhakikishia watu haki zao za kimsingi. Kukiwepo amani watu huweza kutangamana na kutagusana bila uoga. Wanajamii huwezeshwa kufanya biashara zao bila vizuizi, huku wakiheshimiana wakubwa kwa wadogo, viongozi kwa wafuasi, matajiri kwa wakata. Umoja huvuta watu na kuwaleta pamoja wakaweza kushirikiana ili kufikia malengo yao ya kibinafsi na ya kitaifa. Huchangia maendeleo na ujazo wa kitaifa. Umoja huimarisha amani na upendo katika nchi. Huipa nchi nguvu na nishati ya kupigana dhidi ya maovu ya kijamii kama vile ufisadi, ukabila na unyanyasaji.

Maridhiano ni mapatano yanayotokea baada ya makundi au makabila kuwa na mafarakano au vita. Maridhiano huleta pamoja makundi yaliyo hasimu na kupitia mazungumzo ya uhakika na ukweli, makundi hayo husameheana na kuzitupa tofauti zao katika kaburi la sahau. Wanajamii huanza tena kuthaminiana na kuheshimiana. Kwa hivyo, mgombea Uhuru anapotaja hizi dhana tatu, anafahamu namna ambavyo zinaathiri wasikilizaji wake. Anaelewa kwa jinsi gani zinawagusa hasa wale walioathiriwa na vita vya baada ya uchaguzi mwaka wa 2007. Angependa wapiga kura wamwone kama mwokozi kwa kuwa bila kuwepo hayo, hawawezi kupiga hatua yoyote ya maendeleo.

Ingawa uneni wake ni wa kukosha na wenye kutoa matumaini makubwa, kizungumkuti ni kuwa haelezi namna atakavyohakikisha kuwa haya yametekelezwa, wala hasemi, akipata uongozi, ni lini atayatekeleza. Kuna wasiwasi kuwa huenda haya ayasemayo yakabaki ndoto tu kwenye kumbukizi za wapiga kura. Mchakato wa kuleta maridhiano ni changamano mno na si wa kuzungumziwa kiholela. Kadhalika, hakuna uhakika kuwa anachokimaanisha kupitia maneno haya ni sawa na kile wanachokielewa wasikilizaji. Hali halisi ni kuwa maana mwafaka ya maneno haya ni zibwe. Maana halisi hutegemea ni nani anayaeleza. 'Uhuru' na 'utumwa' huweza kumaanisha kitu kimoja kwa watu tofauti kutegemea muktadha, nia na wapi msemaji amesimama.

Mfano wa tatu :

> *Nafikiri haikubaliki kamwe kuwa tunalazimika kama nchi kushauriana kuhusu Migingo wakati Uganda, nchi rafiki imekitwaa ... Bila shaka nitatuma jeshi la wanamaji, kwa bahati nzuri Uganda haina jeshi la wanamaji. Nitakichukua kisha tushauriane baada ya kuwaambia Waganda wanaokikalia kimakosa waondoke halafu kazi ya usoroveya iendelee.*
> Muite, Awamu 1, (1:31:18)

Hili ni suala linalohusu usalama wa kitaifa. Wananchi hupenda kuishi wakijua kuwa usalama wao umehakikishwa na uongozi ulio mamlakani. Ni hatari na ni madharau kuvamiwa na wanajeshi wa nchi jirani na kutwaliwa sehemu ambayo wananchi wanaona ni halali yao. Hali hii ndiyo inayozunguka kisiwa cha Migingo. Walipoulizwa kama kisiwa cha Migingo kiko katika mipaka ya Kenya, wagombea wote walisema 'ndiyo'! Hata hivyo, nukuu hii kutoka kwa Muite inaonyesha kiwango cha jazba aliyo nayo kuhusu kisiwa cha migingo. Anataka wapiga kura waone alivyo shupavu. Swali tunalouliza ni je, jazba hii ni ya mdomo tu ama inatoka ndani ya roho ya mgombea huyu? Kwake anaona ni fursa nzuri ya kujipigia debe kwa kuonyesha hadhira kuwa yeye ni mzalendo aliye tayari kuifia nchi yake na kamwe hataruhusu yeyote kuhatarisha usalama wa nchi au kutwaa mali yake.

## Hitimisho

Utafiti ulitambulisha matumizi ya mikakati ya Ubandikaji jina na Majumlishi memeto. Ubandikaji jina au uvunjiaji heshima ulitumiwa na wagombea kuhusisha wapinzani wao ama mawazo yao na ishara hasi kwa matumaini kwamba hadhira ingewakataa wapinzani au mawazo yao kwa misingi ya ishara hasi zilizohusishwa nao. Ujumlishi memeto ulitumika na wagombea kwa kutoa kauli au maneno ambayo, ingawa kijuujuu yalionekana kumetuka, ndani yake hayakuwa na mashiko yoyote. Matamshi ya wagombea yalionekana kuwa ya thamani na faafu kwa nje lakini yalipochunguzwa kwa kina hayakuonyesha kuwepo kwa ukweli wowote.

## MAREJELEO

Babbie, E. (2009) *The practice of Social Research*. Carlifonia: Wardsworth Publishing.

Benoit, W. L. (2009). *The Functional approach to presidential Television Spots: Acclaiming, Attacking and Defending* 1952-2000 . New York: Praeger.
Brownell, J. ( 2016) *Listening: Attitudes, Principles and Skills*. London: Routeledge.
Fairclough, N. na Wodak, R (1997) 'Critical Discourse Analysis' *in* T. Van Dijk (Ed.), *Discourse as a social Interaction,* London: Sage (pp 258-284).
Gal, D.M, Gall, J.P. na Borg W.R. (1996) *Education Research: An Introduction (6th. Ed.).* New York: Longman Publishers.
Halliday, M.A.K (1989) *Spoken and written Language*. Oxford: Oxford University Press.
Howard, J. (1998) *Families* (paperback) New York: Transactional Publishers.
Institute for Propaganda Analysis. (1938) Propaganda Analysis: Volume I of the Publications of the Institute for Propaganda Analysis, Inc. October, l937 to October, 1938. New York: Institute for Propaganda Analysis, Inc.

Irungu, K. (1999) *The Machiavellian Art of Political Manipulation: The Kenyan Experince*. Thika: The House of Hedges.
Joubish, F. (2011) Paradigms and Characteristics of a Good Qualitative research. *World Applied Sciences Journal 12.*
Nwandito, N. (1999) Education research for modern scholars. *4th Nigerian Dimension Publishers.*
Ogilvy, D. 1963) *The Confessions of Advertising Man*. New York: David Ogilvy Trustees.
Oruodho, A.J. (2003) *Essentials of Education and social science research methods.* Nairobi: Masola publishers.
Patton, M. (1990) *Qualitative Evaluation and Research Methods*. Beverly Hills: Sage. *http//legacy.oise.utoronto.ca/research/field-centres/ross/ctl1014/patton1990.pdf29/10/2015*
Paxon, W.C (1985) *Principles of Style for the Business Writer*. New York: Dodd, Mead and Company.
Pekka, I. (2011) Analyzing Presidential Debates: Functional Theory and Finnish Political communication culture. *Nordicom Review 32 pp 31-43*.
Ropeik, D. (2012) How tribalism overrules Reason, and Makes Risky Times more dangerous. *Bid Think*
Shabo, M. E. (2005) *Techniques of propaganda and Persuasion*. Clayton: Prestwick House.
Smith, J. (2003) Manipulation of The People: The Rudiments of propaganda. *www.energygrid.com/media/2003/09ap-manipulation.html.*
Szanto. G. (1978) *Theatre and Propaganda*. Texas: University of Texas Press.
The Kenya Presidential Debate 2013.